

# *BASI MACHO YAO YALIFUMBULIWA*

## *NAO WAKAMTAMBUA*

¶ Katika Injili ya Luka Mtakatifu, na kuanzia sura ya 24 na ile ya thelathini... kifungu cha 31, ama nitasema kifungu cha 30 cha sura ya 24.

*Ikawa alipokuwa ameketi nao chakulani, ndipo akatwaa mkate, akaubariki, akaumega, akawapa.*

*Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua; kisha akatoweka mbele yao.*

*Wakaambiana, Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi, njiani, na kutufunulia maandiko?*

<sup>2</sup> Na Bwana aongeze baraka Zake. Somo langu lingekuwa, kama ningeliita usiku wa leo: *Basi Macho Yao Yalifumbuliwa Nao Wakamtambua*. Sasa kuna joto, lakini natamani ungevumilia tu uwezavyo, kwa dakika chache tu, nami nitajaribu kuharakisha. Lakini sasa tunataka kuangalia kwa dhati Neno, Neno la ajabu la Mungu. Na tunaomba ya kwamba Mungu, kwa njia fulani, atayafumbua macho yetu usiku wa leo.

<sup>3</sup> Ikiwa Pasaka ni sherehe tu ya tukio la kihistoria, na hilo pekee, basi tuna sababu kidogo ya kuwa na shaka, tuna sababu kidogo ya kuhoji, kwa sababu ingeachwa juu ya wazo zito la kuchukua tu neno. Na kama Kristo hangefanya ahadi alizofanya, basi sisi pia, tusingekuwa na ushahidi tulio nao.

<sup>4</sup> Lakini Bwana wetu mbarikiwa alisema, alipokuwa hapa duniani, "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena." Sasa neno hilo *ulimwengu* hapo, linatokana na "utaratibu wa dunia, watu wa dunia." "Ulimwengu hautaniona tena. Lakini ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Sasa, Maneno hayo ni ya kweli tu kama Maneno mengine yoyote ambayo tumenena kupitia juma hili, kutoka kwenye Biblia, ni kweli tu kama Maneno mengine yoyote katika Biblia. "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena. Hawatafunguliwa macho yao kamwe." Kuna watu ambao wamezaliwa ulimwenguni, si kwa mapenzi ya Mungu, lakini kwa chaguo lao wenywewe la ubinafsí hawangemwamini kama angalikuwa amesimama papa hapa akizungumza nanyi usiku wa leo. Inasikitisha kusema, lakini Biblia ilisema kwamba, "Walizaliwa katika ulimwengu huu, kwa hukumu hii," Yuda, na yapata aya ya 3.

<sup>5</sup> Sasa, lakini kwenu, usiku wa leo, mnaokuja na kusimama chumbani, na kukusanyika pamoja katika jengo dogo lenye joto kali namna hii, hamkuja ili tu kuonekana. Mmekuja kwa kusudi fulani. Na, kwa maoni yangu, umekuja na unyofu wa moyo wako, kwa ajili ya kutembea karibu na Mungu, kuondoka hapa, usiku wa leo, mtu bora kuliko ulivyoomba ulipoingia. Hivyo ndivyo nilivyoomba nilipokuwa nikiingga mlangoni, usiku wa leo, “Bwana, nifanye mtu bora zaidi ninapotoka, usiku wa leo, kuliko nilivyo ninapoingia.” Sasa wakati Yeye . . .

<sup>6</sup> Kabla ya kuondoka Kwake, alitoa matamshi ya namna hii. Alisema, “Yeye aniaminiye Mimi . . .” Yohana Mtakatifu, sura ya 14, kifungu cha 7. “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye naye atazifanya pia; nyingi kuliko hizi atafanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu. Ninakwenda, na kuja tena.”

<sup>7</sup> Sasa tutapata kazi alizofanya. Kazi alizofanya? Hakujidai kuwa mtu mkuu, alikuwa ni Mtu mnyenyeketu tu. Hakuzungumza kwa msamiati wowote wa hali ya juu, alizungumza tu kama Mtu wa kawaida. Aliishi kati ya maskini, “mbweha walikuwa na mapango, na ndege walikuwa na viota, lakini Yeye hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake.” Alikuwa na vazi moja, alilopewa, “lilikuwa limefumwa kote, bila mshono ndani yake.”

<sup>8</sup> Hiyo ndiyo sababu walilipigia kura. Kwa nini ilikuwa hivyo? Kwa sababu unabii wa Agano la Kale ilibidi litimizwe, “Waligawana nguo Zangu, wakapigia kura vazi Langu.” Kwa hivyo hawakuweza kulipasua kwa mshono, iliwabidi kulipigia kura, na hiyo ilikuwa ni kutimiza unabii wa Agano la Kale.

<sup>9</sup> Lakini tutaona, katika dakika chache tu, Yeye alifanya nini? Nami ninaamini, usiku wa leo, ni njaa ya kila mmoja wa miyo yetu, kutoka mdogo kuliko wote hadi aliye na umri mkubwa kuliko wote, usiku wa leo, kumwona Yesu Kristo. Ni shauku ya moyo wangu. Na ni kwa nini? Ikiwa tunadai kwa Maandiko . . .

<sup>10</sup> Redio zinaitangaza leo, televisheni zinaweka vipindi, michezo ya kuigiza imesema, kwamba, “Hayupo hapa, lakini amefufuka!”

<sup>11</sup> Vema, basi, kama amefufuka, Biblia ilisema, katika Waebrania 13:8, “Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.” Sasa, hapa ndipo ilipo, jamani. Hiyo ama ni Kweli, au si Kweli. Kwamba, kama hiyo si Kweli, basi Biblia ni ya uongo, halafu Maneno ni ya uongo; na basi tumepotea, na hakuna ufuuo wa wafu, nasi tunajifanya tu kuamini. Lakini kama ni Kweli, basi haina budi kujithibitisha Yenyewe.

<sup>12</sup> Ukisemaji haya ni maji, sijawahi kuona maji hapo awali, ukiyamimina juu yangu, na hayaloweshi, basi ma—maneno yako si ya kweli, lakini ikiwa unayamimina juu yangu, nayo yanaloguesha, basi maneno yako ni kweli.

<sup>13</sup> Ikiwa Kristo ni ye ye yule jana, leo, na hata milele, basi Biblia ni kweli. Kama Yeye si yule yule jana, leo, na hata milele, basi si kweli. Kama Maneno ya Mungu si ya kweli, basi Kristo si wa kweli. Basi, kama Maneno ya Mungu si ya kweli, Mungu si wa kweli. Lakini, basi, ikiwa Neno la Mungu ni kweli, basi Biblia ni kweli, Mungu ni wa kweli, Kristo ni wa kweli, nasi tunapaswa kuwa waaminifu kwa Huduma. Kweli!

<sup>14</sup> Sasa, alipokuwa duniani, hakudai kuwa mponyaji ye yote mashuhuri. Ni wangapi wanaojua Mwana wa Mungu hakuwahi kudai kuwa mponyaji? Kweli kabisa. Alisema, “Siwezi kufanya neno Mwenyewe, ila kile ninachomwona Baba akifanya. Si Mimi nifanyaye hizo kazi,” alisema, “ni Baba akaaye ndani Yangu. Yeye huzifanya hizo kazi.” Alifanya kazi za aina gani?

<sup>15</sup> Tunaona katika Biblia, ambapo jamaa mmoja jina lake Filipo aliokolewa. Naye akaenda na kumkuta rafiki, Nathanaeli, huko nyuma, maili thelathini nyuma ya mlima. Akamrudisha kwa Yesu. Naye alipomkuta, alikuwa chini ya mti, akiomba. Naye akasema, “Njoo, umwone Yule tuliyempata: Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu.”

Akasema, “Je, kunawenza kuwa na jambo lolote jema kutoka Nazareti?”

Akasema, “Njoo uone.”

<sup>16</sup> Huo ndio ushahidi bora zaidi niujuao. Usichukue neno la mtu mwininge kwa ajili Yake. Njoo, ujionee mwenyewe! Kasema, “Njoo uone.”

<sup>17</sup> Basi alipokuja, Yesu alikuwa amesimama kwenye mstari, labda akiwaombea watu. Ndipo Filipo alipopanda, pamoja na Nathanaeli, Yesu alisema, “Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!”

<sup>18</sup> Akasema, “Ulinijua lini, Rabi?” Ilimshangaza. “Umenijulia wapi Wewe?”

<sup>19</sup> Akasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nalikuona.” Umbali wa maili thelathini, kupitia mlima, hata hivyo, “Nilikuona.”

<sup>20</sup> Hiyo ilionyesha Yeye alikuwa ni Nani. Alikuwa ni Mungu aliye kila mahali; si nabii tu, bali Mungu Mwenyewe aliyedhihirishwa katika mwili. Hiyo ndiyo sababu angeweza kuuweka, uhai Wake, chini, autwae tena.

<sup>21</sup> Maskini mwanamke mmoja alitoka kuja kuteka maji siku moja. Naye akanena naye, na kusema, “Mwanamke, niletée maji ninywe!”

<sup>22</sup> Mwanamke akasema, “Si desturi kwenu Wayahudi kutuumba sisi, Wasamaria, kitu kama hicho. Hatuna uhusiano kati yetu.”

<sup>23</sup> Yeye akasema, "Lakini kama ungalijua ni Nani ulikuwa ukisema naye, ungeniomba Mimi maji unywe. Ningekuletea Maji usije hapa kuteka."

<sup>24</sup> Naye akasema, "Kisima ni kirefu, Bwana. Huna chochote cha kuchotea, basi unaweza kupata wapi Maji haya."

<sup>25</sup> Yeye alikuwa akifanya nini? Akiwasiliana na roho yake. Naye alipopata shida yake ilikuwa nini, shida yake ilikuwa kwamba alikuwa akiishi katika uzinzi. Alikuwa na waume watano, na alikuwa akiishi na wa sita.

Basi Yesu akamwambia, "Nenda, kamwite mume wako, na mje hapa."

Naye akasema, "Sina mume yeoyote."

<sup>26</sup> Akasema, "Hapana, umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa si wako. Kwa hiyo, umesema vema."

<sup>27</sup> Tazama sasa, Myahudi. Yesu alipomfanyia muujiza huo, yule Myahudi kwelikweli, Myahudi wa halisi, wa kweli, kasema, "Wewe ni Mwana wa Mungu, Mfalme wa Israeli." Alijuwa ya kwamba ishara hizo zilipaswa kuandamana na Masihi.

<sup>28</sup> Na sasa huyu hapa Msamaria. Wakati muujiza huo ulipofanyika juu yake, alisema, "Bwana, naona kwamba Wewe ni Nabii. Tunajua ya kwamba Masihi atakapokuja, Yeye atatuambia mambo haya. Lakini Wewe ni Nani?"

Akasema, "Mimi ninayesema nawe Ndiye."

<sup>29</sup> Akaacha mtungi wake wa maji, akakimbilia mjini, na kusema, "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?" Hakika.

<sup>30</sup> Kupitia Maandiko tungeweza kuichukua, jinsi Yeye alivyofanya mambo ambayo Baba alimwonyesha. Biblia ilisema, kule katika Yohana Mtakatifu, walipomhoji kuhusu kwa nini Yeye hakuwaponya wale watu wote vilema, na Yeye akasema, "Amin, amin, nawaambia." Yohana Mtakatifu 5:19, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezি kutenda neno Mwenyewe; ila lile ambalo Yeye amwona Baba analitenda, hilo atenda Mwana vile vile."

<sup>31</sup> Sasa, ikiwa Kristo amefufuka kutoka kwa wafu, na yuko kati yetu leo; na akaahidi kwamba mambo yale yale aliyofanya, kwamba sisi pia tungefanya; hiyo ama ni Kweli, au si Kweli. Biblia ilisema, "Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele."

<sup>32</sup> Na, marafiki, nina furaha kujua, leo, kwamba mimi kweli, pamoa na yote yaliyo ndani yangu, naamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Alichukuliwa mimba na kuzaliwa, kuzaliwa safi. Aliteseka chini ya Pontio Pilato; akasulubiwa, akafa, akazikwa, akafufuka tena siku ya tatu; na akapaa Mbunguni, na ameketi mkono wa kuume wa Ukuu Wake. Naye

Roho Mtakatifu yuko hapa akiendelea na kazi ile ile aliyofanya alipokuwa hapa duniani. Ni wazo zuri jinsi gani!

<sup>33</sup> Ni asubuhi nzuri jinsi gani, asubuhi ya kwanza ya ufufuo, Pasaka ya kwanza ambayo imewahi kupambazuka duniani! Je, unatambua ya kwamba Pasaka hii tunayo adhimisha, ya kufufuka Kwake, inaelekeza tu kwenye Pasaka kuu inayokuja, saa ambayo Yeye atakuja kutoka Mbinguni? Na wote waliokufa katika Kristo watafufuka na kwenda pamoja Naye. Tunatazamia tu hiyo, Pasaka kuu inayokuja. Na, leo, jinsi ilivyo nzuri, ni faraja iliyoje, ni thibitisho jinsi gani tulilo nalo, wakati Biblia inapoitangaza, wakati kuwepo kwake kila mahali kunapotangaza jambo hilo, wakati Nguvu Zake za uponyaji zinapotangaza jambo hilo, wakati Roho Wake mkuu anapotangaza jambo hilo, wakati kila kitu katika maumbile kikitangaza, Kanisa Lake hulitangaza, moyo wangu hulitangaza, kila moyo wa mtu aliyezaliwa mara ya pili hutangaza, ya kwamba, “Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, na atakuja tena! Na Yeye ni yule yule sasa, ‘Jana, leo, na hata milele!’” Sasa angalia.

<sup>34</sup> Ilikuwa kwenye asubuhi hii nzuri ya Pasaka. Kulikuwa na uvumi mwangi, mazungumzo. Baadhi ya wanawake walikuwa wamerudi kutoka kaburini, na wakasema waliona ono la Malaika. Na walidhani ni mtunza bustani; Mariamu, mama, kwa maana alisikia sauti ikisema nyuma yake, ikisema, “Unamtafuta nani?” Na alipogeu...

<sup>35</sup> Aligeuka na kusema, “Wamemuondoa Bwana wangu. Sijui wamemweka wapi. Kama unajua, niambie alipo, nami nitaenda kumchukua.”

Akageuka, na akasema, “Mariamu.”

<sup>36</sup> Naye akamtazama, akasema, “Raboni,” ambayo inamaanisha, “Mwalimu!”

<sup>37</sup> Akasema, “Msiniguse, kwa maana sijapaa bado. Lakini nitapaa kwenda kwa Baba yenu, na kwa Baba yangu, kwa Mungu wangu, na kwa Mungu wenu. Lakini nendeni, mkawaambie wanafunzi Wangu nitakutana nao Galilaya.”

<sup>38</sup> Jinsi hiyo ilivyoonekana kuwa hadithi ya upuuzi, ya Mtu huyu ambaye walimwona akitiwa dawa; na akafa, akazikwa, na hii ilikuwa siku ya nne, ama siku ya tatu tangu alipokuifa. Petro alikuwa amekata tamaa, na alitaka kwenda kuvua samaki. Wawili kati yao wakasema, mmoja jina lake Kleopa, akasema, “Tutarudi tu nyumbani, Yerusalem.” Na wakiwa njiani, wakitembea, asubuhi hiyo, Petro alipochukua kamba yake ya uvuvi na kuondoka kwenda kuvua samaki, wawili hawa walikuwa njiani, wamehuzunika. Nao walipokuwa wakienda njiani, wakisema, “Kweli, nadhani maisha hayafai kuishiwa. Loo, jinsi tulivyoamini ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi! Mtu huyo, aliywafufua wafu, angeweza je kusimama na

kumwacha kuhani huyo mkuu amdhihaki? Ingekuwaje Mtu huyo, Ambaye angeweza kuona ono baada ya ono, kumwacha askari wa Kirumi amfunge kitambaa usoni Mwake, na kumpiga kichwani, na kusema, ‘Ikiwa Wewe ni nabii, tuambie ni nani aliyekupiga?’ Angewezaje kupiga kelele kuomba rehema, msalabani, akiona ya kwamba angeweza hata kuwafufua wafu?’’ Loo, ilikuwa wakati wa kufisha moyo!

<sup>39</sup> Na nyakati hizo za kufisha moyo zinamfikia kila mwaminio, ili kukujaribu, na kukujaribu, na kuona kama kweli unaamini. “Kila mwana anayekuja kwa Mungu, lazima kwanza ajaribiwe, afunzwe kitoto.”

<sup>40</sup> Kutakuwa na baadhi yenu hapa usiku wa leo, hapana shaka, watakaoptia majaribio yale yale. Kama tukiitisha mstari wa maombi, sijui ni nani walio na kadi za maombi, hakuna mtu mwingine anayejua; zote zilichanganywa tu pamoja, na kukabidhiwa kwenu. Nitaita kutoka mahali fulani, popote palipo mawazoni mwangu wakati huo. Hatuwezi kusimama ila wachache kwa wakati mmoja. Dazeni kadhaa, labda, watapita kwenye mstari wa maombi. Wote wanataka kuja. Unaweza kufikiri kwamba amekupita, lakini hajakupita. Anakujaribu tu, akiona tu kama kweli utamwamini. Ono haliponyi; ono huthibitisha tu Uwepo Wake.

<sup>41</sup> Nilikuwa tu nimeketi hapa, nikitazama sasa hivi kote kwenye hadhira. Nami naona ra—rafiki yangu, Bibi Cox, kutoka huko chini Kentucky. Alikuwa na kansa kubwa usoni mwake, majuma machache yaliyopita, ilikuwa imekwisha kula kabisa karibu na jicho lake. Alikuwa yuafa. Bibi Wood, rafiki yangu mwema, alinipigia simu, naye alikuwa analia, akasema, ‘‘Ninaamini itakula jicho la mama kabisa, katika siku chache.’’ Daktari alianza kuichezea, na aina fulani ya vitu, na kuitawanya. Ilikuwa katika hali mbaya sana. Nikaingia na kutoa maombi mafupi, rahisi, pamoja na imani iliyotiwa nanga, ya kwamba ingetendeka. Naye huyu hapa ameketi hapa usiku wa leo, mzima kabisa na mwenye afya; hakuna hata doa lake lililosalia, yote imeponywa, usoni mwake. Ameketi papa hapa mbele yetu. Wengine karibu, wakiwa na kitu kile kile. Kwa nini? Ni kwa sababu Yesu Kristo alifufuka kutoka kwa wafu, Naye yu hai.

<sup>42</sup> Yule yule aliyeweza kumgusa mwenye ukoma, na kusema, “Ninataka, uwe safi,” anaweza kugusa kansa na kusema, “Ninataka, uwe safi,” kama ni ye ye yule jana, leo, na hata milele.

<sup>43</sup> Na Kleopa na wao walipokuwa wakitembea, wamevunjika moyo, walikuwa kwa namna fulani katika mojawapo ya asubuhi hizo zenye huzuni, ikionekana kana kwamba kila jambo linakwenda mrاما. Ndipo ghafla, Mtu fulani akatokea, alipokuja nyuma yao, akatembea na kuwafikia. Nao hawakujua

kwamba huyo alikuwa ni Bwana Yesu! Alikuwa hai, na watu wengi waliompenda hawakujua.

<sup>44</sup> Na hiyo ni sawa na ilivyo leo. Kuna watu wengi leo wanaompenda Bwana, nao hawatambui. Unaweza kuwaambia juu yake, na hata hivyo hawawezi kutambua ya kwamba yu hai hata milele, usiku wa leo, ya kwamba yuko hapa katika kanisa hili usiku wa leo, kwamba Yeye yuko katikati yetu, na atakuwepo mpaka atakapokuja katika mwili, wa kawaida. “Sitakuacha wala sitakupungukia.”

<sup>45</sup> Na walipokuwa wakienda na kuanza kuzungumza njiani, Yesu, nataka uone jambo la kwanza alilofanya Yesu, alienda moja kwa moja kwenye Maandiko, akasema, “Ewe, mpumbavu wa moyo, ni vigumu kwako kuamini yale waliyosema manabii?” Kwa maana, alikuwa ndio kwanza awaulize, “Mbona mmehuzunika sana?”

<sup>46</sup> Nao wakasema, “Kwani Wewe ni mgeni? Hivi hujui ya kuwa Yesu wa Nazareti, Yule tuliyemdhania kuwa ndiye Masihi, Mkombozi wa Israeli, hivi hujui ya kuwa hii ni siku ya tatu tangu asulubiwe? Naye alikuwa ni Mtu hodari katika Neno. Alikuwa Nabii hodari, kwa maana miujiza mingi na kadhalika, Mungu alifanya kupitia Yeye. Na hii ni siku ya tatu; na sasa wamemwua, na kumzika, Naye alikuwa kaburini. Na baadhi ya wanawake walikuja kwetu na katuambia kwamba amefufuka kutoka kwa wafu. Nasi tulijua ilikuwa tu ni hadithi ya kipumbavu, kwa hiyo tuko njiani kurudi.”

<sup>47</sup> Hapo ndipo alipoanza kulifungua Neno. Loo, ninalipenda Neno la Milele la Mungu! Akaanza kupitia Maandiko, kuanzia kwa Musa. Yeye kamwe hakuacha chochote bila kushughulikiwa, alienda moja kwa moja kwenye Neno!

<sup>48</sup> Mtu yejote aliyetumwa na Mungu, sijali yeye ni nani, atadumu na Neno la Mungu. Asipofanya hivyo, yeye si mtumishi wa kweli wa Mungu.

<sup>49</sup> Alienda moja kwa moja kwenye Neno. Naye alionyesha, kwa Neno, ya kwamba Kristo alipaswa kufa, kufufuka tena, na kuingia katika Utukufu Wake. Sasa, loo, jinsi hapana shaka walizungumza!

<sup>50</sup> Ningetamani kuwa na mazungumzo hayo ya saa chache Naye (nawe je?) njiani. Unasema, “Vema, Ndugu Branham, hakika ningetamani. Laiti ningeweza.” Naam, tunaweza kuwa nayo sasa hivi. Huyo ni Yeye akizungumza na wewe, moyoni mwako. Hutambui tu.

<sup>51</sup> Sasa angalia alipokuwa akiukaribia mji, jioni ilikuwa inakuja, alioneekana kana kwamba anaenda kupita.

<sup>52</sup> Anaweza kukufanya hivyo, pia. Anaweza kukufanya ufikiri ya kwamba ataendelea, lakini hatapita. Hatapita. Anataka tu umwalike Yeye.

<sup>53</sup> Wakamwambia, “Loo, siku imeenda sana. Sasa usiendelee, lakini tafadhali ingia na ukae nasi.” Wewe mpe tu mwaliko wa namna hiyo, uone kitakachotukia. Akasema, “Siku imeenda sana sasa, njoo ukae nasi. Ni karibu jioni.” Kisha akageuka na kuingia, kwenye mkahawa huo mdogo, nyumba ndogo ya wageni.

Huko Ulaya bado wanayo. Unakula na kulala, na kila kitu kinalipwa kwa bili moja, hoteli yako.

<sup>54</sup> Na alipoingia nao ndani! Hii hapa sehemu nzuri. Siku hiyo yote, walipokuwa wakizungumza Naye, Yeye kamwe hakusema jambo moja. Hata hivyo, walikuwa wametembea pamoja Naye na kuzungumza Naye, hapo awali, lakini hawakutambua.

<sup>55</sup> Ni nani aliyekuepushia ajali siku ile? Ni nani aliyemfanya mtoto yule apone? Ni nani aliyekulipia ile bili ya mboga? Ilikuwa ni Yeye, lakini hilitambui. Ni nani aliyekupa afya kuja kanisani usiku wa leo? Ni Yeye, lakini hilitambui. Loo, laiti tungefanya tu kama wao, tumwalike tu aingie ndani!

<sup>56</sup> Na alipoingia, akaingia ndani, akafunga milango, ndipo akafanya jambo ambalo hakuna mtu mwingine angeweza kulifanya hivyo. Yeye Ndiye pekee ambaye angeweza kufanya jambo hilo, kwa maana walikuwa pamoja Naye kabla ya kusulubiwa Kwake. Naye akautwaa mkate huo, na, jinsi tu alivyoufanya, hiyo ilikuwa ni njia Yake Mwenyewe ya kufanya jambo hilo. Ndipo macho yao yakafunguka, nao wakajua huyo angeweza tu kuwa ni Yeye. Hakukaa nao muda mrefu sana. Akatoweeka machoni pao, kwa muda mfupi tu. [Ndugu Branham alidata vidole vyake—Mh.]

<sup>57</sup> Na walipokuwa njiani, walirudi mbio kadiri walivyoweza kwenda, upesi, wakipiga kelele za ushindi tu, kuwaambia kuwa, “Bwana amefufuka kweli!” Hawakurudi kubishania dini yao. Hawakurudi kubishana juu Yake. Lakini walijua tu kwamba alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu!

<sup>58</sup> Sasa, marafiki, kama Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai, baada ya miaka elfu moja na mia tisa iliyopita, kama Biblia ni kweli, alisema, “Mimi ni hai milele na milele,” Yeye yu hai hapa, katika jengo hili usiku wa leo, kama alivyokuwa siku ya kufufuka Kwake, Yuko kwenye mwili tu.

<sup>59</sup> Baadhi yao walikuwa wamekusanyika pamoja. Naye akaja moja kwa moja kupitia kuta, akatokea moja kwa moja ndani, katikati yao, akasema, “Hapa, niguseni. Tazameni makovu Yangu mikononi Mwangu. Je, roho ina nyama na mifupa kama nilivyo nayo?” Akasema, “Nipe chakula.” Nao wakampa samaki na mkate. Naye akasimama pale na kukila, mbele yao, akasema, “Roho hali kama mnavyoniona Mimi ninakula.”

<sup>60</sup> Yeye ni kitu gani? Yeye ni yule Yehova Mungu mkuu aliye hai, ambaye yuko katikati yetu usiku wa leo. Yuko katikati popote wakusanyikapo wawili au watatu: “Nitakuwa katikati yao.”

<sup>61</sup> Na sasa hivi ndivyo ninavyofikiria. Ikiwa Kristo atakuja kwenye kusanyiko hili la watu, huku ukitokwa na jasho, ukingoja, na atathibitisha, kwenye Pasaka hii, ya kwamba Yeye yu hai, na amesimama katika jengo hili usiku wa leo, basi unayo haki ya kumwomba Yeye chochote alichofia, na kuamini ya kwamba utakipokea. Je, unaamini hiyo kuwa ni Kweli? Bila shaka, ni kweli.

<sup>62</sup> Sasa, ningeweza kuzungumza nanyi kwa muda mrefu, lakini Neno moja kutoka kwa Kristo litamaanisha zaidi ya maneno yote ningeweza kusema; nimechoka na kukakamaa katika sauti, na mchovu kama iliyvo katika sauti.

<sup>63</sup> Na halafu jambo lingine, katika kunena. Ni vigumu, kwa kuwa hapa ni nyumbani kwangu, kuwa na mkutano wenyewe mafanikio na upako wa Roho namna hiyo. Kwa nini? Kwa sababu hapa ni nyumbani kwangu. Yesu alisema kwamba, “Nabii, katika nyumba yake mwenyewe, nchi yake mwenyewe, hata katika wilaya yake mwenyewe.” Ni kitu tu kinachotokea kwa njia hiyo.

<sup>64</sup> Walisema kwamba alipokwenda nyumbani Kwake Mwenyewe, walisema, “Huyu si mwana wa seremala? Si mama Yake, Mariamu, yupo hapa pamoja nasi? Si ndugu Zake wote wako hapa, na dada Zake? Si tunawajua? Alitoka shule gani? Je, alikuwa mhitimu wa seminari gani? Ni stakabadhi gani alizo nazo?” Naye hakupitia shule yoyote ama seminari yoyote, ama vitambulisho vyovyote, bali Yeye alitoka kwa Mungu. Lakini hawakuweza kuiona. Walisema, “Anapata wapi hekima hii?”

<sup>65</sup> Na walipomwona akitambua mawazo hayo ya watu, Petro alipomjia, Yeye alisema, “Jina lako ni Simoni, jina la baba yako ni Yona,” ilimitatiza. Alimjuaje Yeye?

<sup>66</sup> Mafarisayo walisimama karibu, wakasema, “Yeye ni Beelzebuli. Yeye ndiye mkuu wa wapiga ramli. Yeye ni ibilisi!”

<sup>67</sup> Naye Yesu akasema, “Mkisema hayo juu Yangu, Mwana wa Adamu, mtasamehewa. Lakini Roho Mtakatifu atakapokuja na kufanya jambo lilo hilo, nawe ukana neno moja dhidi Yake, hutusamehewa kamwe, katika ulimwengu huu au ulimwengu ujao.” Kwa hiyo, ni jambo la hatari. Basi Yeye alijuaje? Kwa nini alisema hivyo? Alijua ya kwamba ishara hizo zingekoma mpaka siku hizi za mwisho.

<sup>68</sup> Na siku hizi za mwisho, Yeye hangekuwa mwenye haki, kumwaga ghadhabu Yake juu ya watu wenyewe haki. Wana... Sisi tumpemba katika mizani, na kuonekana tumpungukiwa. Yote tunayofikiria ni burudani, programu za redio, ambazo hazijadhibitiwa, Elvis Presley, Arthur Godfrey, maskini vichekesho vichafu, watu mashuhuri wa redio na televisheni. Tunakaa nyumbani Jumatano usiku, mbali na mkutano wa maombi, kuona uozo kama huo, na kujiita Wakristo?

<sup>69</sup> Halafu Mungu anapomwaga Roho Wake, na kuonyesha ishara za kufufuka Kwake, tunamhukumu na kuondoka. Na hiyo ni dhambi isiyosameheka, kufanya hivyo. Yesu alisema, “Nena neno moja dhidi Yake, halitasamehewa kamwe, katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao.” Kwa hiyo Roho huyo hana budi kuja katika siku hizi za mwisho, kuthibitisha hilo Neno la Mungu kuwa ni kweli.

<sup>70</sup> Nami ninasema, chini ya mamlaka ya Neno la Mungu, na hisia ya nafsi yangu mwenyewe: Roho Mtakatifu yuyo huyo (Roho) yuko papa hapa sasa katikati ya watu hawa. Sasa, nilidai ya kwamba amefufuka kutoka kwa wafu. Nilidai yu hai, yu hai milele. Nilidai Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele; yule yule katika kanuni, yule yule katika Nguvu; yule yule katika kila jambo, yote isipokuwa mwili Wake wa kawaida unaoketi mkono wa kuume wa Mungu na Ukuu, katika Utukufu. Lakini Roho Mtakatifu yuko hapa, akifanya kazi, akisonga, akitenda, akifanya sawa kabisa kama Yesu Kristo alivyofanya, kwa kuwa ni thibitisho la kufufuka Kwake. Ni saa nzuri jinsi gani! Sasa nadhani mnaona mahali ninaposimama.

<sup>71</sup> Sasa, si tu na maskini watu hawa, yapata watu mia moja, ama mia mbili hapa katika—katika jengo hili dogo, waliosongamana humu usiku wa leo, lakini nimetoa kauli hiyo mbele ya maelfu mara maelfu, na mamia ya maelfu, nimeshika Biblia kwa mkono mmoja, na Korani kwa mkono mwagine, nikasema, “moja ni sahihi, na nyininge si sahihi,” na kusahi kila kuhani wa Kiislamu kuja na kuthibitisha, au mwagine yejote, Buddha, au chochote awezacho kuwa, dhidi ya Korani, na dhidi ya dini yao, lakini kila mtu anakaa kimya.

<sup>72</sup> Lakini, ndugu, sababu ya mimi kufanya hivyo, kwa sababu ninajua Mkombozi wangu yu hai! Na Yeye ndiye Kweli. Yesu Kristo yu hai. Yuko hapa!

<sup>73</sup> Sasa si chochote ndani yangu ambacho ningeweza kufanya, ni karama ya Mungu. “Je, unaifanyaje?” Ni kujisalimisha tu.

<sup>74</sup> Moja kwa moja katika jengo hili sasa kuna Malaika wengi, sana. Unasema, “Je, hayo ni Maandiko?” Hiyo ni Biblia. Ngoja nikuonyeshe. Ni Wakristo wangapi walio hapa? Inua mkono wako. Vema, unaweza kuziandika. Biblia ilisema kwamba, “Malaika wa Mungu wamepiga kambi kuwazunguka wale wamchao.” Basi, kuna Malaika hapa!

<sup>75</sup> Halafu Kristo alisema, “Popote walipo wawili au watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, nitakuwa katikati yao.” Basi, Yeye yuko hapa! Jambo pekee ni kwamba, huwezi kumwona, bali kwa imani tunaliamini.

<sup>76</sup> Ninaweza kukuthibitishia kuwa redio inapitia hapa, pia, sauti. Ninaweza kukuthibitishia kuwa picha zinapitia hapa. Haitapiga kwenye bomba *hili* hapa; haitapiga *hiki*, kioo *hiki*, kwenye maikrofoni hii; wala haitaingia kwenye kipande *hiki* cha

nyenzo, maana haikutengenezwa hivyo. Lakini kuna kipande cha nyenzo ambacho kitazalisha tena hiyo picha.

<sup>77</sup> Na Mungu aliweka wengine katika Kanisa, kwanza mitume, kisha manabii, waalimu, wainjilisti, na wachungaji, yote kwa ajili ya kulikamilisha Kanisa. Tungeweza kumkataa mmoja, na kusema huyo mwininge siye? Mungu hufanya jambo hilo, Mwenyewe. Si kitu ulimwenguni ila kujisalimisha tu kwa Roho Mtakatifu. Naye Roho Mtakatifu huchukua mamlaka kutoka hapo, nawe hujui unachofanya. Ni kazi kuu ya Roho Mtakatifu.

<sup>78</sup> Sasa, marafiki, mji wangu wa nyumbani. Nami nataka kusema hili sasa, kabla ya kufunga uamsho huu. Moja ya siku hizi hakutakuwa na hata majivu kidogo yatakayosalia Jeffersonville, hakutakuwa na hata moja litakalosalia Charlestown, hakutakuwa hata moja litakalosalia Louisville. Ulimwengu huu uko tayari kwa hukumu. Wana bomu la haidrojeni sasa ambalo Urusi inaweza kurusha kutoka Moscow, ikatua kwenye Barabara ya Nne, na kuchukua kila moja ya mimea hii ya unga hapa, na kuizamisha futi sabini na tano chini ya ardhi, kwa bomu moja. Bomu moja; maili kumi na tano mraba, itaenda hadi futi mia moja na hamsini ardhini. Mkono uko juu ya kifyatua risasi. Saa inayoyoma. Muda umeenda kuliko unavyodhania. Kwa nini kusubiri hadi wakati huo?

<sup>79</sup> Kumbuka, "Maskani hii iliyo ya dunia ikiharibika, tunayo moja tayari inayongoja." Usiogope mabomu ya haidrojeni wala kingine chochote. Maadamu una Kristo moyoni mwako, hilo ndilo kimbilio bora zaidi la bomu njualo. Limetengenezwa kutokana na manyoya; chini ya mbawa Zake, unadumu. Kwa hiyo usijali kuhusu mambo hayo, kama wewe ni Mkristo.

<sup>80</sup> Lakini kama wewe si Mkristo, bila shaka umesimama mahali pabaya. Hujui ni dakika gani moyo wako utaacha kupiga. Biblia ilisema watu watakuwa katika siku za mwisho, kwa shida ya moyo, "Moyo wa watu unazimia, hofu, kuchanganyikiwa kwa nyakati, dhiki kati ya mataifa." Angalia ni nini zaidi, wanaume wanakuwa wengi mara kumi, zaidi ya wanawake; Biblia haikusema kamwe miyo ya wanawake itazimia, ilisema, "Miyo ya wanaume itazimia." Ni kabisa, kikamilifu.

<sup>81</sup> Hivi majuzi kule Oakland, mimi na mke wangu tulikuwa kule San Francisco, lile tetemeko kuu la ardhi lilitikisa. Na ardhi ikaanza kutetemeka kwa nguvu na kuyumba pale, mpaka majengo yakatikisika, na dohani zikaanguka. Mipira mikubwa ya hewa ilipanda namna *hiyo*, ikiwa na moshi ndani yake, ama masizi, chochote ilichokuwa, kutoka sehemu hizo. Na watu wakakimbilia mitaani, wakipiga mayowe. Nikawazia, "Itakuwaje wakati Bwana atakapotokea kweli?" Vilabu vyahome, moja kwa moja, wakirudisha pombe zao, kwenye rafu, na kuziuza. Watu wanaingia kuinunua. Mtu huyo hangeweza kuiuza ikiwa hakuna mtu aliyeinunua. Hiyo ni kweli.

<sup>82</sup> Ni, sisi ndio wenye hatia. Hebu nikwambie, ndugu. Mimi ni Mmarekani, na ninaipenda nchi yangu. Lakini taifa hili la kale limepimwa katika mizani, na kuonekana limepungukiwa. Linazama, hakika kama mimi nilivyo mhudumu nyuma ya jukwaa hili usiku wa leo. Sasa nasema hivyo ili kupata kibali kwa Mungu. Nasema hivyo kwa sababu Mungu ameiweka moyoni mwangu niiseme. Na jambo bora zaidi kwako kufanya ni kujitayarisha kwa ajili ya Kuja kwa Bwana.

<sup>83</sup> Sasa mwaminini Yeye, iweni na imani Kwake. Sasa, maneno yote ningeweza kusema, nasema tena, hayangemaanisha kitu kimoja kwa kile ambacho Yesu angesema. Lakini unatambua mahali ninaposimama, pamoja na kundi hili la watu usiku wa leo? Ama nimekatiza vibaya, nimetafsiri vibaya jambo fulani, ama nimesema Kweli. Sasa kama Yesu Kristo amefufuka kutoka kwa wafu, na, aliahidi, mambo yale yale aliyofanya tungefanya pia, nami nimedai, kutoka kwa mtoto mdogo wa kiume . . .

<sup>84</sup> Sikuwa na umri wa miezi kumi na minane, nadhani, lakini si zaidi ya miaka miwili, hata hivyo, nilipoona ono langu la kwanza. Imekuwa, maisha yangu yote. Watu hapa maskanini, wanajua jambo hilo. Muda wote ambao nimekuwa hapa, hakuna wakati mmoja ambapo imewahi kushindwa. Na haitashindwa kamwe, maana ni Mungu. Ulimwenguni kote imeenda, uamsho mkuu umezuka. Na sasa, kwa neema ya Mungu, niko katika milioni yangu ya pili ya nafsi, moja kwa moja kwenye mkutano wangu, nikiwaleta kwa Bwana Yesu. Milioni ya pili, hiyo ni kweli. Na hebu fikiria tu mamilioni mengine ambao wametoka, Oral Roberts, hizo cheche zote ambazo zimewashwa kutokana na jambo hilo, na kuendelea, maelfu mara maelfu, mpaka ulimwenguni kote kuna uamsho mmoja mkubwa sana wa Nguvu za Mungu, unaoendelea. Naye ibilisi anaachilia kila aina ya mambo ya uongo, ili kuzipinga. Lakini Neno halisi la kweli la Mungu, litaenda moja kwa moja hadi mwisho. Halitashindwa kamwe! "Mimi Bwana, nimeipanda. Nitaimwagilia maji mchana na usiku, wasije baadhi ya watu kuinyakua kutoka mkononi Mwangu."

<sup>85</sup> Sasa, usiku wa leo, nilidai ya kwamba Kristo alifufuka kutoka kwa wafu. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Sasa, Bwana awabariki. Kama Yeye atafanya hivyo, basi wewe ni . . . Ikiwa unaamini, Mungu akubariki. Mwulize, basi, atakapokuja jukwaani. Ikiwa Kristo atatokea hapa kwenye jukwaa hili! Hapa kuna changamoto. Ikiwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, atatokea papa hapa jukwaani, na kufanya mambo yale yale aliyofanya Yeye alipokuwa hapa duniani, utamwamini?

<sup>86</sup> Mwangalie Yeye, akiwa njiani kuelekea Emau, jinsi hao wavulana, walivyovunja . . . Alipoumega mkate huo, alifanya jambo fulani pale ambalo hakuna mtu mwingine angeweza kufanya. Lilikuwa ni jambo ambalo Kristo peke yake angeweza kufanya. Nao walilitambua.

<sup>87</sup> Sasa kama atafanya jambo lile lile hapa, ambalo Kristo peke yake anaweza kufanya; si jambo fulani la uongo, bali ni jambo lile lile alilofanya Yeye; basi mwaminini, mpokeeni, iweni na imani Kwake, mpendeni, mumtumikie.

<sup>88</sup> Hebu niwaambieni, usijiunge tu na kanisa sasa. Hiyo haitafanikiwa. Huna budi kuzaliwa mara ya pili. Si kuchochaea hisia; si kitu fulani kidogo ulichosema, “Vema, nilipaza sauti. Nilinenya kwa lugha. Nilifanya *hivi*,” hilo silo. Wakati chini kabisa moyoni mwako, Kitu fulani kinakuja kukubadilisha, nawe unakuwa kiumbe kipyä katika Kristo Yesu; ulimpokeea Mtu, Kristo Yesu; mambo ya kale yanapokufa, na mambo mapya yanazaliwa tena; unasahihisha mambo, ambayo ulifanya makosa; unawapenda adui zako, unawaombea wale wanaokutumia vibaya; hapo ndipo unapokuwa Mkristo. Mti hujulikana kwa matunda unaozaa.

<sup>89</sup> Bwana na awabariki sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu. Nitamwomba dada aende kwenye piano,acheze taratibu “Yule Tabibu mkuu sasa yu karibu, Yesu mwenye huruma.” Na ninyi mlío nje, sasa, mlío na kadi za maombi, songeni karibu na mlango, tutaanza baada ya muda mfupi. Na tuombe.

<sup>90</sup> Baba yetu wa Mbinguni Mbarikiwa. Loo, sauti yangu mbaya, miezi minne ya kuzungumza, nimechoka sana kwa sauti yangu. Lakini ninaomba ya kwamba Wewe utanisaidia sasa hivi. Hapa kutakuwa na hatua nyingine muhimu kwenye Maskani ya Branham. Hapa atatokea shahidi mwingine katika siku za mwisho, kwenye Siku ya Hukumu. Wengi wamesimama ndami na nje, usiku wa leo, wengi wao wanashangaa, wengi wanawazia, “Je, ni kweli, au si kweli?”

<sup>91</sup> Ee Baba wa Milele na Mbarikiwa, tunaomba ya kwamba sasa utadhihirisha upendo Wako kwetu, kwa kuonekana hapa na kulifanya Neno Lako kuwa kweli. Nimenena juu ya Neno Lako; kama ulivyofanya, Mwenyewe, kwa Kleopa na rafiki yake, wakielekea Emau. Na tukiwa njiani, Bwana, tunaposafiri, Wewe sema nasi kupitia Neno Lako. Na sasa njoo kati yetu! Ee Kristo Mkuu, njoo mionganoni mwetu, thibitisha Maneno Yako kuwa kweli, na udhihirishe Uwepo Wako hapa usiku wa leo. Kama, sisi viumbé maskini tuisostahili tunapokiri kwamba sisi ni wenye dhambi na hatustahili mambo haya, lakini tunayaamini, Bwana. Na kwa neema tunayakubali, kwa njia ya imani, ya kwamba tumeokolewa, na ni watoto Wako. Tubariki sasa, Bwana.

<sup>92</sup> Ninajua Neno Lako ni kweli, uliposema juu ya “nabii katika mji wake mwenyewe, kati ya watu wake mwenyewe.” Lakini, Bwana, naomba, kwa ajili ya usiku huu tu, ya kwamba Wewe utawatazama tu watu hawa, na ujidhihirishe Mwenyewe kwa mara nyingine tena hapa katika jiji hili, kupitia huduma ya Roho Mtakatifu. Ee Mungu wa Milele, utubariki sasa tunapokungojea Wewe. Na ufanye mambo uliyofanya kabla ya

kusulubiwa Kwako, na Jeffersonville haitakuwa na hata jambo moja la kulalamikia. Lakini, tunajua ya kwamba hawatakuwa na udhuru Siku ile, kwamba umejidhihirisha Mwenyewe. Katika Jina la Yesu, ninaomba. Amina.

<sup>93</sup> [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . si kile anachotaka niombee. La, si kansa, kwa maana ameponywa hiyo. Lakini anataka niombee shida ya mgongo aliyo nayo. Hiyo ni kweli. Ni shida mgongoni mwake. Je, hiyo ni kweli? Sasa unaamini alifufuka kutoka kwa wafu? Sasa tazama. Nikizungumza naye kwa muda mrefu zaidi kidogo, labda jambo lingine litasemwa. Sijui. Sasa, sikujuia shida yako ni nini. Sijui sasa ilikuwa ni nini. Unaona? Lakini warekodishaji wanayo, unaweza kupata kile Yeye alisema.

<sup>94</sup> Hebu tuzungumze zaidi kidogo tu, na tuone kama Yeye ataniambia jambo lingine. Ninaona mwanamke ambaye anaonekana kitu kama . . . Ni mwanamke mwingine, naye anamwombea. Naye yuko katika namna fulani ya taasisi au hospitali, ni kitu kama . . . ni mahali pa magonjwa ya akili. Ni Madison, Indiana. Ni—ni—ni da—dada ambaye unamtakia maombi, ambaye yuko kwenye taasisi. Na ikiwa utaamini kwa moyo wako wote, na yote yaliyo ndani yako, Mungu atakukomboa na kuponya mgongo wako na kukupa afya. Unaamini sasa? Vema, njoo hapa.

<sup>95</sup> Mpendwa Baba wa Mbinguni, tunaomba ya kwamba katika Jina la Yesu Kristo, ya kwamba utamponya mwanamke huyu, na kumfanya mzima. Na umpe baraka hii. Nami naomba ya kwamba rehema za Mungu ziwe juu yake, na zitamponya, na kujipatia Mwenyewe utukufu. Ninaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

<sup>96</sup> Naweza kusema hivi. Kuna mtetemo unaotoka pale, kutoka papa *hapa* nyuma. Hebu kidogo tu, simama hapo kwa dakika moja. Niliona kuwa Nuru hiyo ilikuacha. Kuna wengi sana, wamejaa sana karibu na mimi hapa. Kila mtu ana-vuta. Lakini ninaiona ikienda kwako. Ni mtu fulani ambaye . . . Una—una upasuaji wa kike unaotarajiwa. Hiyo ni kweli. Niliona watu wawili ama watatu wakitokea, na ile Nuru ikayumbayumba moja kwa moja pale nyuma na kumpiga mtu huyo aliyesimama moja kwa moja pale nyuma. Ni wao wanaombea hilo. Unaona? Hiyo ni kweli. Na unayo, ni hali ya mwanamke ambaye amefanyiwa upasuaji wa kike. Hiyo ni kweli. Sasa nenda ukapokee uponyaji wako, na Bwana Mungu akakuponya. Amina.

<sup>97</sup> Je, waweza kuja? Huyo mama, je, unamwamini Bwana Yesu? [Dada huyo anasema, “Ndiyo, bwana.”—Mh.] Je, unaamini kwamba alifufuka kutoka kwa wafu? Sasa, kukujuia wewe, sikuju. Labda nimekuona ikiwa unatoka karibu hapa. Sijui. Watu huja na kuondoka, siko karibu na maskani hapa vya

kutosha kujua. Lakini, wewe, unatoka mjini? [“Ndiyo.”] Unatoka mjini. Vema, basi, lakini sikujui. Lakini Kristo anakujua. Lakini kama atanifunulia, nikisimama hapa, kilichokuleta hapa, utaamini na kukubali hicho? Na unajua sijui uko hapa kwa sababu gani, sina fununu. Jambo pekee, unaweza kuwa umeniona mjini, ama kitu fulani, ama, ama chochote kile. Sijui. Hiyo ni juu ya Mungu ku—kujua hilo.

<sup>98</sup> Huko nyuma kabisa, unataka kuondokea tatizo hilo la utumbo ambalo umekuwa nalo? Je, unaamini Bwana Yesu atakuponya? Ikiwa unaamini, unaweza kuwa nao.

<sup>99</sup> Mwingine ana hesabu mbaya ya damu, ameketi kule nyuma, niliwaona wakichukua. Je, unaamini Bwana atakuponya? Vema. Je, unaamini kwa moyo wako wote? Basi unaweza kupata uponyaji wako, Mungu alikuponya wakati uo huo. Ulimgusa Yeye. Hukunigusa mimi, uko umbali wa futi thelathini kutoka kwangu. Amina.

<sup>100</sup> Sasa unaamini amefufuka kutoka kwa wafu? Angalia tu, na uishi, sasa wakati mstari unasonga. Loo, ni vigumu sana hapa Jeffersonville! Unaona? Na umati kama huu karibu nawe, kila mtu! Yesu alimshika mtu mkono, akampeleka nje ya mji, wakati mmoja.

<sup>101</sup> Sasa angalia huku, dada, kwa muda kidogo tu. Amini kwamba Bwana Yesu yupo kukusaidia. Unasumbuliwa na shida ambayo iko kwenye rektamu, na daktari amekuchunguza. Naye alikuambia ilikuwa ni bawasiri. Ninakuona pia ukijaribu kutembea nyumbani, na unakwenda polepole sana. Una baridi yabisi. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.<sup>1</sup> Daktari alisema ni lazima ufanyiwe upasuaji. Hiyo ni kweli kabisa. Nami nimewona akiitia saini kadi hiyo ndogo pale ofisini mwake: Rebekah Baker, 509 Barabara ya Graham. Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ni ofisini kwake, kwenye kumbukumbu. Hiyo ni kweli. Unaamini? [Dada huyo anasema, “Ndiyo, bwana.”—Mh.] Basi unaweza kupata uponyaji wako. Katika, Jina la Bwana Yesu Kristo, jalia mwanamke huyu apokee uponyaji wake. Amina. Mungu akubariki, mama. Nenda, ukiamini sasa. Uwe na imani kwa Mungu.

Laiti ungeweza tu kutambua Uwepo wa Bwana!

<sup>102</sup> Sasa mama anayesimama hapa, ili mweze... Sikujui wewe, nijuavyo mimi. Wewe hunijui, na mimi sikujui. Je, hiyo ni kweli? Vema. Basi wewe ni mtu ambaye hunijui, na mimi siwajui. Na sikumjua yule mama mwininge. Lakini mama huyu ni mgeni kabisa, nijuavyo mimi. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, mama. Mara yetu ya kwanza kuwahi kukutana, maishani.

<sup>103</sup> Hawa hapa mwanamke na mwanamume. Picha nzuri tu ya Yohana Mtakatifu 4, ambapo mwanamke na Mwanaume walikutana; na mwanamke huyo alikuwa Msamaria, Yesu alikuwa Myahudi. Na wakaanza kuongea wao kwa wao, ndipo

Yesu akafunua siri za moyo wake na kumjulisha ilipokuwa shida yake. Sasa, ikiwa Yeye ni Yesu yeye yule leo, anaweza kufanya kazi iyo hiyo leo.

<sup>104</sup> Ikiwa mwanamke huyu atainua mkono wake kwa Mungu, si kuapa (kwa sababu, hatuamini kufanya hivyo), ainue tu mkono wake kwa uaminifu, pamoja na wangu, kwamba hatujawahi kuonana hapo awali, na hatujui chochote mmoja kuhusu mwenzake. Je, utainua mkono wako, mama? Haya basi. Hajawahi kuniona, au sijawahi kumwona, na yeye ni mgeni kabisa. Sasa ikiwa kuna . . .

<sup>105</sup> Uwepo wa Bwana Yesu uko hapa. Ikiwa mwanamke huyo ni mgonjwa, singeweza kumponya. Tayari ameponywa; Kristo alimponya alipokufa kwa ajili yake. Je, unaamini hilo? Lakini kama angalikuwa amesimama hapa sasa, akiwa na . . . mahali ninaposimama, na Yeye angeweza, angeweza kumfunulia, au kufanya jambo fulani ili kuinua imani yake kukutana! Sasa, anaweza kuwa amesimama hapa kwa sababu ya matatizo ya kifedha. Anaweza kuwa amesimama hapa katika matatizo ya nyumbani. Huenda amesimama hapa, akifa kwa kansa. Anaweza kuwa amesimama hapa akiwa na TB. Sijui. Siwezi kusema.

<sup>106</sup> Na sasa ukitaka kujiweka katika nafasi yangu, njoo hapa na uchukue nafasi yangu, umekaribishwa. [Ndugu Branham anatulia—Mh.] Hakika. Wala sijui, wala singefanya hivyo. Lakini Mungu wa Mbinguni anajua. Unaweza kuelewa sasa?

<sup>107</sup> Na kama Kristo atafanya jambo lile lile hapa, ile Kweli isiyoweza kukosea, kama vile alivyofufuka kutoka kwa wafu, na kuthibitisha ya kwamba Yeye ni Yesu yeye yule aliyezungumza na yule mwanamke kisimani, ni wangapi humu ndani wanasesma, “Nitampokea sasa hivi kama Mponyaji wangu, ama chochote ninachohitaji”? Inua mkono wako, useme, “Nitampokea kama atafanya hivyo.”

<sup>108</sup> Mwanamke huyo aliyeinua mikono juu, hatujawahi kukutana. Bwana alijalie, ndilo ombi langu. Sasa huyo mama anaonekana kusogea kutoka kwangu; ikiwa wasikilizaji wanaweza kuisikia sauti yangu. Naona mtu amesimama. Sio kwa ajili yake mwenyewe, sana. Anamwombea mtu mwingine, na huyo ni mama mkongwe. Ni mama yake, anamwombea. Hiyo ni kweli. Ana mishtuko midogo ya moyo, kutetemeka kidogo kwa moyo, kitu kama hicho. Hawezi kulala usiku. Hiyo si ni kweli? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Naye huyo mama hatoki katika nchi hii. Huyo mama anatoka mbali na hapa. Mwanamke huyo anatoka Georgia. Hiyo ni kweli kabisa. Na unatoka Georgia. Nawe unataka maombi kwa ajili ya jicho lako, pia. Unakuwa kipofu machoni mwako. Na hiyo ni kweli. Je, unaamini Mungu atakuponya? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema.

<sup>109</sup> Sasa unaamini? Sasa uwe na imani katika Mungu. Ninapomwombea, jiombee huko nje, na umwamini Mungu. Yuko hapa, yuko kila mahali.

Njoo hapa, dada.

<sup>110</sup> Mwokozi mbarikiwa, ninaomba ya kwamba, katika Jina la Kristo, ya kwamba utamjalia mwanamke huyu shauku yake. Jalia Nguvu za Mwenyezi Mungu zikae juu yake, na jalia aponywe na kupata kile alichoomba. Ninaomba baraka hii katika Jina la Yesu. Amina.

<sup>111</sup> Sasa nenda, ukishangilia, na mwenye furaha. Na uamini, dada, na upone. Vema.

<sup>112</sup> Sina hakika, lakini ninaamini ninamfahamu mwanamke huyu. Ninaamini unatoka Georgetown, kwa sababu mimi ni... Si wewe ni jamaa wa Ndugu Arganbright? Bila shaka, sasa upako huu, ni tofauti. Unatambua kuwa kuna tofauti sasa hivi. Ninapozungumza nawe mahali pengine; ni tofauti sasa hivi. Ulihisi hisia ya kupendeza sana, kitu kama hicho. Ni Roho Mtakatifu. Huko hapa kwa ajili yako mwenyewe. Uko hapa kwa ajili ya mtu mwengine, na huyo ni msichana mdogo wa karibu miaka minne au mitano. Ana shida ya figo, naye anaishi kaskazini mwa Indiana. Hiyo ni kweli. Kitu hicho ulicho nacho mkononi mwako, umpelekee, naye atapona. Amini kwa moyo wako wote sasa, na upokee ulichoomba, katika Jina la Kristo.

“Ikiwa unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana!”

<sup>113</sup> Huyu hapa mwanamke ambaye ni mgeni kwangu. Sikuui, sijawahi kukuona maishani mwangu. Sisi ni wageni mmoja kwa mwenzake, tumeachana kwa miaka mingi; labda mingi, tumezaliwa umbali wa maili nydingi. Sikuui, sijawahi kukuona. Lakini Yesu Kristo anakujua.

<sup>114</sup> Kitu kilitokea katika kusanyiko; mtu alionekana karibu nami. Huyu hapa ameketi, papa hapa, kitovu kilichopasuka. Je, unaamini, bwana? [Ndugu huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Basi Kristo anakuponya na kukupa afya! Amina.

<sup>115</sup> Hiyo ndiyo njia ya kulifanya, amini! Aligusa nini? Sijawahi kumwona mtu huyo; lakini aliponywa papo hapo. Alimgusa Bwana Yesu Yule aliyepo hapa. Ondoa kutokuamini huko kwako! Sahau kuhusu mimi kuwa William Branham. Mwangalie Yesu Kristo, Yeye Ndiye aliye hapa. Ninaisahi imani yako, katika Jina la Kristo, kusahau kunihusu mimi; na kuamini ya kwamba huyu ni Bwana Yesu hapa, na uone kitakachotukia. Sijali uko wapi kwenye jengo hili.

<sup>116</sup> Sasa huyu hapa mwanamke mdogo. Sijawahi kumwona. Ana umri mkubwa kuliko mimi. Yeye, sijui yeye ni nani, anatoka wapi, sijui chochote kumhusu. Mimi ni mgeni kabisa kwake. Lakini Kristo anamjua.

<sup>117</sup> Kama atanifunulia kile kilichokuleta hapa, je, utakipokea na kukiamini? [Dada huyo anasema, “Hakika.”—Mh.] Ulikuwa na hisia ya ajabu dakika chache zilizopita, nilipozungumza jambo fulani, sivyo? Ilikuwa dada yako aliye katika hospitali ya wendawazimu huko Madison, Indiana. Hiyo ni sahihi. Kwa maana, mwanamke mwininge alikuwa amesimama hapa, nawe ulikuwa umesimama pale ukiangalia moja kwa moja upande huu. Na lile ono, ulikuwa unaamini ulipokuja. Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ndiyo iliyoifanya. Na sababu ya wewe kuwa hapa usiku wa leo, ni kwa sababu una shida ya moyo. Ndiyo kwanza uwe na mshtuko wa moyo. Hiyo ni kweli kabisa. Nami naona sasa, ninapotazama katika ono, ile nchi yenye kuyumbayumba. Unatoka mahali fulani hapa kusini mwa Indiana. Unatoka karibu na Corydon, ndiko unakotoka. Rudi nyumbani, umepona. Yesu Kristo anakuponya. Hiyo ni ROHO MTAKATIFU ASEMA HIVI.

<sup>118</sup> Kuwa na imani, na uamini. Usiwe na shaka. Amini tu. Je, unaweza kutambua kuwepo kila mahali kwa Bwana Yesu? Ajabu ilioje! Kuna nini?

<sup>119</sup> Hapa kwenye kona, naona ono. Daktari hajui kama ni kansa au TB. Hiyo ni kweli. Lakini kama utaliamini, umeponywa, hata hivyo. Imani yako imekuokoa. Endelea.

<sup>120</sup> Haya basi. Kuwepo kila mahali kwa Mungu aliye hai! Ninaipa changamoto imani yako. “Kama unaweza kuamini!” Sasa, amefufuka kutoka kwa wafu. Yuko hapa pamoja nasi. Huyo Ndiye! Hayo ndiyo mambo yale yale aliyofanya alipokuwa hapa duniani. Miaka elfu mbili imepita, Yeye bado yu hai, na yu hai milele na milele. Amini tu, kuwa na imani.

<sup>121</sup> Sikujui, mama. Sijawahi kukuona maishani mwangu, sijui chochote kukuhusu. Hiyo ni kweli, sivyo? Yesu Kristo anakujua. Ikiwa Mungu atanifunulia kilichokuleta hapa, utamwamini, na kuniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Kama atafanya hivyo, unajua Kitu fulani kimenitia upako. Ungepaswa kujua ni Hicho. Sasa kama ningesema, “Nitaweka mikono yangu juu yako, upone,” ungekuwa na haki ya kutilia shaka hilo. Lakini kama Mungu akiniambia jambo fulani unalojua kuwa ni kweli, basi unajua kama hiyo ni kweli ama si kweli. Je, hiyo ni kweli? [Dada huyo anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Ni ugonjwa wa kike. Imefanyiwa upasuaji, nakuona ukitoka kwenye meza ya upasuaji, ukiwa na kitu cheupe juu ya uso wako, lakini haukufanikiwa. Hiyo ni kweli. Lakini, huyo ibilisi alijificha daktari asimwone, lakini hawezi kujifichia Mungu. Nenda nyumbani, ukawe mzima, mama, Yesu Kristo amekuponya na kukupa afya.

Ikiwa unaweza kuamini!

<sup>122</sup> Mimi ni mgeni kwako, mama. Je, unaamini kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yuko hapa? Unaamini atakuponya?

Kisukari si kitu, kwa Mungu kuponya. Unaamini atakuponya? Basi nenda nyumbani ukapokee uponyaji wako, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Amina.

Njoo hapa, mama. Unaamini?

<sup>123</sup> Sasa acha kuwaza hayo huko nyuma! Sio “telepathia.” Huwezi kupita nayo sasa! Ngoja nikuonyeshe.

<sup>124</sup> Simjui mwanamke huyu. Weka mikono yako juu ya yangu, mama. Ikiwa Mungu atanifunulia shida yako ni nini! Ninaangalia upande *huu*, unajua sisomi akili yako. Kama Mungu atanifunulia shida yako ni nini, je, utaamini Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, nami ni mtumishi Wake? Kama utaamini, inua mkono wako. Una shida ya kike, shida ya mwanamke. Hiyo ni kweli. Ulikuwa nayo; huna sasa. Umepona. Nenda zako, na ufurahi na kushangilia.

<sup>125</sup> Njoo, bwana. Maskini tatizo hilo la figo, na jambo fulani linalokusumbua. Je, unaamini Mungu atakuponya? [Ndugu huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Akuponye huo? Basi, katika Jina la Yesu Kristo, pokeea uponyaji wako, na uende zako, ukishangilia. Amina. Mungu akubariki, ndugu.

Amini!

<sup>126</sup> U hali gani, mama? Hivi hungependa kwenda, kula chakula kizuri tena kama ulivyokuwa ukifanya? Umekuwa na wasiwasi sana, sivyo? Ilisababisha kidonda cha tumbo kuwa tumboni mwako. Nenda, ukajipatie sambusa ya nyama ukale, Yesu Kristo amekuponya. Nenda zako, ukishangilia.

<sup>127</sup> “Kama unaweza kuamini!” Uwe na imani kwa Mungu. Unaamini? Kristo aliye hai, mwenye uwezo wote yuko hapa sasa, kuponya kila mtu hapa ndani.

<sup>128</sup> Hebu kidogo. Huko nyuma kabisa kwenye mstari, anayeketi papa hapa chini, ameketi kijana. Imani yako ni kubwa kuliko vile ulivyofikiri ulikuwa nayo, mwanangu. Ulikuwa na shida ya moyo, sivyo? Ikiwa hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako. Yesu Kristo alikuponya, mwanangu. Uko mzima. Nenda zako, ukawe mzima.

<sup>129</sup> Je, unamwamini? Uwe na imani katika Mungu.

<sup>130</sup> Hapa kuna mwanaume nisiyemjua. Hatufahamiani mmoja kwa mwingine. Ninaamini mtu huyu alibatizwa asubuhi ya leo. Lakini sikuju, sijui chochote kukuhusu. Je, hiyo ni kweli? Ikiwa Yesu Kristo atanifunulia kilichokuleta hapa, utakubali?

<sup>131</sup> Je, ni wangapi katika wasikilizaji wataipokea sasa hivi? “Kama unaweza kuamini!” Kuwa tu na imani. Üsiwe na shaka.

<sup>132</sup> Mwanamume huyo ana shida ya ngozi. Hiyo ni kweli. Nami naona unakuwa... Ni shida ya tezi dume, pia. Hiyo ni kweli. Ikiwa ndivyo, punga mkono wako. Na ninaona kitu cheusi kimesimama kati yako na mwanamke fulani; ni mkeo.

Unamwombea. Yeye ni mwenye dhambi, na unamtaka awe Mkristo. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli. Nenda, uweke mikono yako juu yake, na umwombee, kwamba Mungu aliye Mbinguni atafunua umuhimu wa mambo haya ambayo ni halisi.

<sup>133</sup> Unaamini? Je, unaamini ya kwamba Mungu atafanya jambo hilo? “Kama unaweza kuamini!” Ninaipa changamoto imani yako. Huko nyuma kabisa, popote ulipo, tazama na uishi! Uwe na imani kwa Mungu popote pale ulipo. “Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana.” Kama unaweza kuamini! Tazama, angalia huku, omba.

Unasema, “Unatazama nini, Ndugu Branham?”

<sup>134</sup> Rebekah, rudi hivi kidogo, mpenzi. Simama hapo hapo ulipo. Huyo ni msichana wangu mdogo, ambaye siku moja atakuwa nabii mke, pia. Yule mama aliyesimama hapo karibu nawe, mpenzi, aliyevalia kofia nyeupe, anasumbuliwa na tatizo la uwazi wa pua. Inua mkono wako, ama simama kwa miguu yako, mama. Unaomba kwamba Mungu akuite, anijalie nikuite. Je, hiyo ni kweli? Hebu msichana wangu mdogo akuwekee mikono yake hapo.

Ee Mungu wa Milele, katika Jina la Yesu Kristo, ninakemea huyo pepo anayemsumbuwa mwanamke huyo. Na aondolewe, katika Jina la Kristo. Amina.

<sup>135</sup> Loo, Jina la Bwana libarikiwe! Bwana Yesu na ajifunue Mwenyewe, pia. Je, unaamini Yuko hapa? Basi hebu niwaambie, kila mmoja wenu, sasa hivi, kama mnawenza kuamini, Yesu Kristo anamponya kila mmoja wenu, sasa hivi. Ikiwa maneno yangu ni kweli *hapa*, ni kweli *hapo*. Ikiwa utafanya kile ninachokuambia ufanye, unaweza kuponywa sasa hivi. Je, unaamini hivyo? Basi wekeaneni mikono yenu mmoja juu ya mwingine. Wekeaneni tu mikono yenu ninyi kwa ninyi, ndani au nje. Msitie shaka! Nilisikia roho ya ukiziwi ikiondoka. Huyu hapa, Kristo aliyefufuka!

<sup>136</sup> Ee Mungu wa Milele na Mbarikiwa, katika Jina la Bwana Yesu, natoa changamoto kwa kila roho mchafu, katika Jina la Kristo Bwana, kwamba itaondoka mahali hapa, iwatoke watu hawa. Na jalia Roho Mtakatifu mkuu sasa abatize kila mtu humu ndani, kwa imani kuu ya kuamini.

<sup>137</sup> Ee, Shetani, wewe pepo, umetudanganya vya kutosha. Kristo amefufuka, amesimama hapa akiwa na funguo za mauti na kuzimu zikiwa zinaning’inia juu Yake. Nguvu za uponyaji zimelipiwa. Nasi tunakuapisha, kwa Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai, kwamba uwatoke watu hawa. Toka ndani yao, Shetani, ili waende wakaponywe.

<sup>138</sup> Kama unaamini kwa moyo wako wote kwamba Yesu Kristo alikuponya, simama kwa miguu yako, na ukubali Nguvu za Kiungu za uponyaji za Mwenyezi Mungu. Jambo ndilo hilo!

Bwana asifiwe! Bariki Bwana! Ninyi, kila mmoja, mmeponywa.  
Simama kwa miguu yako, na umpe Mungu sifa! Amina! Jina la  
Bwana libarikiwe! Hebu tumpe Yeye sifa, tunapoinua mikono  
yetu na kumsifu. Abarikiwe Mwana wa Mungu aliye hai!  
Amina!



*BASI MACHO YAO YALIFUMBULIWA NAO WAKAMTAMBUA* SWA57-0421E  
(And Their Eyes Were Opened And They Knew Him)  
MFULULIZO WA UAMSHO WA PASAKA

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili ya Pasaka jioni, tarehe 21 Aprili, 1957, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## **Ilani ya haki ya kunakili**

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

**VOICE OF GOD RECORDINGS**  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)